

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NANYUMBU

Fax No.2510045
Baruapepe: info@nunyumbudc.go.tz
www.nanyumbudc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi
Halmashauri ya Wilaya,
S. L. P. 246,
MASASI-MTWARA

Kumb.Na/NDC/T.20/10/VOL II/18

09/09/2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu anapenda kuwatangazia waombaji wenye sifa nafasi za kazi za **Mtendaji wa Kijiji Daraja la III**.

MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III. NAFASI NNE (04)

Sifa kwa Mwombaji

Awe na elimu ya kidato cha nne (iv) au sita (vi) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/ cheti katika moja ya fani zifuatazo: - Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III

- i. Afisa masuhuli na Mtendaji Mkuu wa serikali ya Kijiji
- ii. Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika Kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mipango ya maendeleo ya Kijiji.
- iv. Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kiongozi wa wakuu na vitengo vya kitaalam katika Kijiji.
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji
- ix. Mwenyekiti wa kikao cha wataalam waliopo katika Kijiji.
- x. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- xi. Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za Kijiji

MSHAHARA

Kwakuzingatia waraka wa mishahara wa Serikali ngazi ya **TGSB1 Tshs.390,000/=** kwa mwezi.


MASHARTI YA KAZI/WAOMBAJI KWA UJUMLA

- Awe Mtanzania
- Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45
- Waombaji ambao ni watumishi wa Umma na wanasifa za kuingilia wapitishe barua zao za maombi kwa waajiri wao.
- Nafasi inayoombwa iandikwe katika kichwa cha habari cha barua.
- Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatuwakuaminika pamoja na namba zao za simu.
- Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma na mafunzo kutoka vyuo vinavyotambuliwa na serikali.
 - Cheti cha kuhitimu kidato cha iv au vi
 - Cheti cha mafunzo ujuzi NTA – level 5
 - Cheti cha kuzaliwa
 - Picha moja “**Passport size**” ya hivi karibuni na iandikwe jina nyuma.
- “Testimonials” “profisional Result” “Statement pf Result” Hati za matokeo ya kidato cha nne na cha Sita (Form iv and Form vi Result slip) **HAVITAKUBALIWA.**
- Waombaji waambatishena nakala ya kitambulisho cha Taifa au Namba ya kitambulisho cha NIDA kwa wasio na kitambulisho.
- Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatishe uthibitisho wa vyeti vyao kutoka Baraza la Mitihani la Taifa (**NECTA NACTE** na **TCU**)
- Uwasilishwaji wa taarifa na sifa za kugushi zitapelekea wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria.
- Waombaji watakaokidhi sifa ndio watakaoitwa kwenye usahili.
- Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au kiingereza na yatumwe kwa njia ya posta au kuwasilishwa moja kwa moja katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu. Sehemu ya masijala ya wazi kwa anuani ifuatayo: -

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),
S. L. P. 246,
NANYUMBU.**

- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 23 Septemba, 2021 saa tisa na nusu (9:30) Alasiri. Tangazo hili linapatikana pia kwenye tovuti ya Halmashauri www.nanyumbudc.go.tz

Tangazo hili limetolewa leo tarehe 09/09/2021 na


Ibrahim J. Mwanauta
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NANYUMBU**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NANYUMBU**